**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA NJOMBE

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe kuomba nafasi za kazi za mkataba zilizotajwa hapo chini kuwasilisha maombi yao.

### 1) MTEKNOLOJIA MIONZI DARAJA LA II(RADIOGRAPHER II ) NAFASI 2

**a) Sifa za kuajiriwa:**

Kuajiriwa mwenye Stashahada katika fani ya mteknolojia daraja la II – Radiografa kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali na ambao wamesajiliwa na baraza (Medical Radiology and Imaging Professional Council)

**b) Kazi na majukumu:**

i. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiotherapia katika eneo lake la kazi
ii. Kutoa huduma ya vipimo kwa wagonjwa wanaoelekezwa eneo lake lake la kazi kwa mionzi sahihi
iii. Kukagua na kusimamia ubora wa mionzi inayotolewa na mitambo ya radiotherapia (Radio – therapetic quality)
iv. Kusimamia watumishi walio chini yake
v. Kutoa ushauri kuhusu kazi za radiotherapia na mionzi katika eneo lake la kazi
vi. Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji katika eneo la kazi (sterilization)
vii. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi
viii. Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

2) MAPOKEZI DARAJA LA II (RECEPTIONISTS II ) NAFASI 3

a) **Sifa za muombaji**

Kuajiriwa mwenye Stashahada katika fani ya mapokezi, Huduma kwa wateja (Customer care services) na mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali

b) **Kazi na Majukumu**

i) Kutunza kumbukumbu sahihi za wagonjwa
ii) Kufuatilia taarifa za mgojwa wodini
iii) Kupokea na kuelekeza wagonjwa juu ya taratibu za matibabu husika
iv) Kupokea na kuelekeza wageni mbalimbali wanaotembelelea Hospital ofisi husika
v) Kuchukua taarifa kutoka kwa mgonjwa
vi) Kutunza siri za mgonjwa (mantain confidentiality)
vii) Kufungua faili za wagonjwa
viii) Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

i) Awe na umri usiozidi miaka 35 na mwenye afya njema
ii) Waombaji waambatishe wasifu (Curriculum Vitae) yenye anwani sahihi, namba za simu sahihi, pamoja na majina mawili ya wadhamini (watumishi wa serikali) na namba zao za simu zinazopatikana
iii) Barua za Wadhamini wawili zikiwa na anwani zao sahihi na namba za simu
iv) Awe na vyeti husika vya Taaluma. Testimonial "provisional results" statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne **HAVIKUBALIKI**
v) Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na TCU au NECTA
vi) Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo vilivyothibitishwa;
   a) Cheti cha kuzaliwa
   b) Cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne
   c) Cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha sita kwa waliohitimu
   d) Cheti cha Taaluma
   e) Picha ya Pasipoti 1
   f) Leseni kutoka mabaraza husika
   g) Cheti cha kompyuta
vii) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **15/08/2025**

Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Posta au moja kwa moja:-

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA NJOMBE
S. L. P. 1044
NJOMBE

**MGANGA MFAWIDHI,**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA NJOMBE,**
**S. L. P 1044,**
**NJOMBE**

***Imetolewa na Ofisi ya Habari na Uhusiano***
***Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe***
***31 Julai 2025***